

Resource: Feed conservation

Media: Farmer radio feature

Type: Interviews/Narration

Date: 04.08.2022

Title__ : Mbinu bora za uhifadhi wa lishe ya ngombe-Silage

CONTROLS: Signature tune, 10 seconds, then down under presenter.

PRESENTER:

Hujambo mpenzi msikilizaji na karibu kwa kipindi kingine cha (Insert name of your program). Kipindi kinachoangazia mbinu bora za ufugaji zinazolenga kuongeza mapato huku utunzi wa mazingira ukizingatiwa.

Jina langu ni(Insert your name)

Kipindi hiki kimetayarishwa kwa ushirikiano kati ya Biovision Africa Trust, Biovision Foundation, Taasisi ya kimataifa ya Utafiti wa Mifugo yaani ILRI na shirika la kimaendeleo ya serikali ya Ujerumani kupitia GIZ.

Kupitia vipindi vya ufugaji , tunaangazia raslimali ambazo wakulima hutumia kusuluhisha changa moto zinazo wakabili katika mashamba yao.

Je, unaweza aje kuboresha ufugaji wa ngombe wakati huu wa mabadiliko ya anga? Ili kujipatia mwongozo wako kuhusu mbinu bunifu za ufugaji wa Ngombe, wasiliana nami kwenye nambari(Insert your studio number).

Nipe jina lako, anwani ya posta nami nitahakikisha kuwa unapokea mwongozo huu.

Insert sfx farm sounds.

Wakulima hufahamu zaidi vile mifugo yao ina adhiriwa na ukosefu wa lishe bora na ya kutosha. Hivyo basi wanaweza kufanya maamuzi jinsi ya kupunguza madhara yanayotokana na ukosefu wa lishe bora kwa mifugo wao.

Wanasayansi nao pia wanavutiwa na mifugo, kimaumbile na mahusiano na lishe bora.

Wanasayansi Taasisi ya kimataifa ya Utafiti wa Mifugo yaani ILRI wanahimiza wakulima kutengeza sileji yaani silage ili kupunguza tatizo la chakula wakati wa kiangazi.

Hapa ni kijijini Kapkuros, County ya Nandi.

Namkuta Mkulima(insert name of the farmer interviewed) na familia yake wakiwa katika harakati za kuvuna mahindi kwa minajil ya kutengeneza silage.

Kila ninapo rusha macho, naona mihindi iliyo shamiri, yenye afya lakini bado haijakauka.

Nimefika hapa kusikiliza na kujifunza juu ya mbinu anazotumia mkulima huyu kukabiliana na ukosefu wa lishe wa ngombe wake wakati wa kiangazi.

Insert Farmer Interview (Why he makes silage)

Namuulizaanajuaje mihindi yake sasa iko tayari kwa kutengeneza silage?

Insert Farmer interview on (How he can tell the maize is ready for silage)

Kishana familia yake wanakusanya mabua ya mahindi yaliyovunwa na kupakia kwenye trakta ambayo linaelekea nyumbani.

Mkulima..... alinieleza kwamba yeye hutengeneza silage yake nyumbani karibu na zizi la ngombe.

Na tunapofika nyumbani, naona tayari kuna watu ambao wana chimba shimo.

Pia naona kando kando kuna panga inatumika.

Naelezwa ni vyema zaidi kutumia mashine ya kukata mabuu ya mihindi kwa vipande vidovidogo.

Kuna mfuko mkubwa wa plastiki.

Hizi bila shaka ndizo zana zitakazo tumika katika kutengeneza silage.

Je, Silage yenyewe inatengenezwa kiviipi? Mkulima.....ako na jibu.

Insert farmer ITW

Je ni mambo yapi unafaa kuzingatia wakati unapotengeneza silage?

- hakikisha maji na hewa haingii ndani ya chakula chako wakati wa kuhifadhi
- utakapo fungua toa kiasi cha kulisha kwa muda huo na kingine endelea kufungia na kuzuia hewa kuingia.
- wanyama wa maziwa wapewe angalau masaa 3 kabla ya kukamua kuepusha harufu katika maziwa.
- silage nzuri itakuwa na kijani na rangi ya ugoro(yaani greenish brown).

Bridge

Ushauri kutoka kwa wakulima wenye uzoefu mkubwa katika ufugaji wa ngombe wa maziwa.

Ukiwa na swali kuhusiana na ufugaji wa ngombe au ungependelea kupata mwongozo kuhusu kuhifadhi lishe ya ngombe wasiliana nami kwenye nambari.....

Jina langu ni

Na kwa niaba ya Biovision Africa Trust tukishirikiana na Biovision foundation, Taasisi ya kimataifa ya Utafiti wa Mifugo yaani ILRI na shirika la kimaendeleo ya serikali ya Ujerumani kupitia GIZ, nakutakia usiku mwema.

CONTROLS: *End tune (10 seconds).*

.....End.....